# MASWALI YA MAANA SANA

I. **"TUTENDEJE, NDUGU ZETU?" MDO. 2:37.**

A. Watu hawa walisikia Injili iliyohubiriwa na Petro, Mdo. 2:14- 36.
B. "Wakachomwa mioyo yao", yaani waliamini wakati walisikia habari, Mdo. 2:37.
C. Kwa swali hili kuu waliambiwa: "Tubuni mkabatizwe kila mmoja kwa jina lake Yesu Kristo mpate ondoleo la dhambi zenu, nanyi mtapokea kipawa cha Roho Mtakatifu," Mdo. 2:38.
D. "Nao waliopokea neno lake wakabatizwa," Mdo. 2:41
E. "Siku ile wakaongezeka watu wapata elfu tatu, Mdo. 2:41.
F. "Bwana akalizidisha kanisa kila siku kwa wale waliokuwa wakiokolewa," Mdo. 2:47. Basi, umemtii Mungu kwa njia ya kufanya mambo haya? Au umefanya njia tofauti na Biblia? Kuokolewa ni lazima kufanya kama tulivyofundishwa na Biblia Utaona njia ya kuokoka kama utachunguza vifungu vifuatavyo kutoka Biblia.

II. **NI NINI KINACHINIZUIA NISIBATIZWE? MDO. 8:36.**

A. Filipo akahubiri Habari Njema za Yesu, Mdo. 8:35.
B. Yule Mkushi akasema, "Tazama, maji haya; ni nini kinachonizuia nisibatizwe?" Mdo. 8:36. Filipo akamjibu, "ukiamini kwa moyo wako wote inawezekana," Mdo. 8:37.
C. Filipo akamjibu, "Ukiamini kwa moyo wako wote, inawezekana," Mdo. 8:37.
D. Mkushi akasema, "naamini ya kwamba Yesu Kristo ni Mwana wa Mungu," Mdo. 8:37.
E. "Wakatelemka wote wawili majini, Filipo na yule Towashi; naye akambatiza," Mdo. 8:38.
F. "Kisha, walipopanda kutoka majini, Roho wa Bwana akamnyakua Filipo, yule Towashi asimwone tena. Basi alikwenda zake akifurahi," Mdo. 8:39. Basi, ubatizo wako sawa sawa na yule mkushi?

Tazama, yule towashi alisikia habari za Yesu na wokovu. Akabatizwa mara moja bila kukawia. Tena ubatizo wake ulikuwa kuzikwa majini, sio kwa kunyunyizia maji usoni.

III. **WAKATI SAULI AKIMLAKI YESU ALIULIZA, "NIFANYE NINI BWANA?" MDO. 22:10.**

A. Tunajua Sauli alikuwa mtu mwaminifu na kutafakari sana mambo ya dini, Mdo. 26:5; Gal. 1:14.
B. Aliliudhi Kanisa. "Akatisha na kuwaza kuwaua wanafunzi wa Bwana," Mdo. 9:1.
C. Alipokuwa akisafiri mpaka Dameski, basi "ghafula nuru kuu ilitoka Mbinguni," Mdo. 22:6.
D. Akaanguka chini, akasikia sauti ikimwambia, Sauli, Sauli, mbona unaniudhi? Mdo. 22:7.

E. Akasema, “Wewe u nani, Bwana,” Mdo. 22:8. Papo hapo Sauli alianza kumwamini Yesu ndiye Mwana wa Mungu.
F. Yesu akasema, “Mimi ni Yesu Mnazareti, ambaye wewe unaniudhi,” Mdo. 22:8.
G. Sauli akasema, “Nifanye nini, Bwana?” Mdo. 22:10. Sauli hajaokolewa bado lakini aliuliza ni lazima afanye nini.
H. Bwana akamwambia, “simama, uingie Dameski, na huko utaambiwa habari za mambo yote yaliyoamriwa uyafanye,” Mdo. 22:10.
I. Sauli “akawa siku tatu haoni; hali, wala hanywi,” Mdo. 9:9. Sauli alikuwa akitubu akangoja kwa habari. Hajaokolewa bado lakini akingoja amri kutoka kwa Bwana.

J. Anania, mtauwa kwa kufuata sheria, akamjia Sauli akasema, “basi sasa, unakawilia nini? Simama, ubatizwe, ukaoshe dhambi zako, ukiliitia jina lake,” Mdo. 22:16.
K. Sauli alisikia habari kutoka kwa Bwana. Akaamini Injili, akatubu dhambi akabatizwa kwa ondoleo la dhambi zake.

Tazama Sauli aliokolewa katika njia moja sawa sawa na watu wa siku ya Pentekoste, Mdo. 2. Na yule Towashi, katika Mdo. 8. Alisikia habari kutoka kwa Yesu. Akaambiwa asimame akabatizwe ili aoshwe dhambi. Hajaokolewa bado, lakini wakati alipobatizwa alipokea ondoleo la dhambi. Ni sawa sawa kwa wakosaji siku hizi. Basi umefanya vilevile sawa na watu hao?

## IV**. “YANIPASA NIFANYE NINI NIPATE KUOKOKA?” MDO. 16:30.**

A. Paulo na Sila walikuwa gerezani katika mji wa Filipi, Mdo. 16:23.
B. “Usiku wa manane Paulo na Sila walikuwa wakimwomba Mungu na kumwimbia nyimbo za kumsifu,” Mdo. 16:25.
C. “Ghafula pakawa tetemeko kuu la nchi, hata misingi ya gereza ikatikisika, na mara hiyo milango ikafungka, vifungo vya wote vikalegezwa,” Mdo. 16:26.
D. “Yule mlinzi wa gereza akaam kanaye alipoona ya kuwa milango ya gereza imefunguka, alifuta upanga, akataka kujiua, akidhani ya kuwa wafungwa wamekimbia,” Mdo. 16:27.
E. “Ila Paulo akapaza sauti yake kwa nguvu, akisema, usijidhuru, kwa maana sote tupo hapa,” Mdo. 16:30.
F. Akataka taa ziletwe, akarukia ndani, akitetemeka kwa hofu, akawaangukia Paulo na Sila akauliza, “Yanipasa nifanye nini nipate kuokoka?” Mdo. 16:30.
G. “Wakamwambia, mwamini Bwana Yesu, nawe utaokoka pamoja na nyumba yako,” Mdo. 16:31. Kitu cha kwanza cha kufanya kwa kila mkosaji ni kumwamini Kristo. Lakini kuna mambo mengine zaidi.
H. “Wakamwambia neno la Bwana, yeye na watu waliomo nyumbani mwake,” Mdo. 16:32. Aliwaeleza mambo ambayo yaliwapasa wajue na wafanye.
I. “Akawakaribisha saa ile ile ya usiku, akawaosha mapigo yao, kasha akabatizwa, yeye na watu wake wote wakati huo huo,” Mdo. 16:33.

Mlinzi aliisikia injili akaiamini akatubu dhambi akabatizwa kwa ondoleo la dhambi zake. Alifanya sawa sawa na watu wengine kwa kuupokea wokovu.

Inatulazimu sisi sote kufanya vile vile sawa na watu hao ili tupokee wokovu!

**Salamu rafiki**:

Kama mtu ameokolewa au amepotea ni kweli jambo la kuishi au kufa.

Mara nyingi swali laulizwa “nifanye nini ili niokoke?” Twaweza kuona jibu lake katika Biblia tu. Twakushauri umkubali kristo kama mwokozi wako ili upokee baraka za neema yake. Usingoje kuhatarisha maisha yako.

Yakubidi kufanya matendo haya: kumwamini Kristo, kutubu dhambi na kutofanya tena, kukiri jina la yesu kristo, kubatizwa kwa ondoleo la dhambi kwa njia ya kuzikwa majini, na kumtumikia Mungu na imani. Ikiwa umekosa kufanya matendo haya au moja wapo, yafaa uyafanye sasa hivi. Tu tayari kukusaidia kwa namna yoyote tuwezayo.

**www.kanisalakristo.com**